BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Nane – Tarehe 09 Mei, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

74. MHESHIMIWA ABDALLA ABAS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiwahimiza wananchi waunde vikundi vya ushirika ili kuweza kuwapatia mikopo nafuu ambapo wananchi wameuitikia wito huo kutoka sehemu mbali mbali kwa hamu na shauku.

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia mikopo wana vikundi hao.

(b) Je, Serikali imevipangia vikundi vingapi kuwapa mikopo kwa mwaka 2021/2022.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

56. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali imeondoa ugatuzi kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi kiutendaji. Hata hivyo, kuna mashaka kwenye mipango inayoaminika ya kuleta ufanisi huo.

(a) Je, Serikali imeandaa utaratibu gani kwa lengo la kupima ufanisi katika Serikali za Mitaa.

(b) Je, wadau husika wa taasisi hizo wameshirikishwa vipi katika kuandaa utaratibu huo.

### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

59. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mnara wa Kigomasha ni moja kati ya maeneo yanayoyoaingizia mapato mengi Serikali kupitia meli mbali mbali zinazopita eneo hilo. Hata hivyo, eneo hilo hadi leo halina maji wala umeme.

Je, kuna sababu zozote zinazopelekea kutoimarishwa kwa eneo hilo ambalo ni muhimu kwa uchumi wetu.

<u>Wizara ya Afya:</u>

42. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na utaratibu wa Wizara ya Afya kupitia vifo vinavyotokea katika hospitali na sababu za vifo hivyo (death review).

(a) Je, ni hatua gani muhimu huchukuliwa baada ya kuvipitia vifo hivyo.

(b) Je, ni mikakati ipi ambayo Wizara imeweka ili kupunguza vifo vya mama na mtoto.

(c) Vifo vingapi vimeripotiwa vya mama na mtoto katika mwaka 2020 – 2021.

63. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) –Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni jambo la kushukuru kwamba, ndani ya jimbo la Wingwi kuna vituo viwili vya afya vinavyotoa huduma za uzazi kwa masaa 24 ambavyo ni Sizini na Wingwi. Hata hivyo inasikitisha kwamba vituo hivyo vina upungufu mkubwa wa wafanyakazi, jambo ambalo linapelekea wafanyakazi hao kubaki vituoni hapo kwa masaa kadhaa kwa ajili ya kutoa huduma na hivyo kupungua kwa ufanisi wao kunakosababishwa na machofu.

(a) Je, kwa nini Serikali imeweka wafanyakazi pungufu katika vituo hivi wakati wafanyakazi wenye sifa na uwezo ndani na nje ya jimbo la Wingwi wapo hata kwa kujitolea.

(b) Je, ni lini Serikali itaviongezea vituo hivyo vya afya wafanyakazi wa kutosha kwa namba na sifa pamoja na kuvipatia walinzi.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

76. MHESHIMIWA MOHAMMED MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali imebahatika kupata fedha za msaada nafuu za Uviko 19 kwa ajili ya uimarishaji wa visima vya maji safi na salama, ambapo kuna mpango wa kununua pampu madhubuti kwa gharama kubwa.

Je, vile visima vilivyokuwa havijabahatika kufanyiwa matengenezo kwa fedha hizo, Serikali itanunua pampu kama hizo kuviendeleza ili wananchi wetu wapate huduma ya maji bila ya usumbufu.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

71. MHESHIMIWA ABDALLA ABAS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali yetu ya awamu ya nane inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi imeunda Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa lengo la kuwainua wananchi kupata ajira hasa wale walio katika ukanda wa bahari.

(a) Je, hadi hivi sasa mwaka 2022 Serikali imefikia hatua gani katika kuwapatia ajira wananchi hao.

(b) Je, ni lini watapatiwa mikopo ya boti na vifaa vyake.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

31. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Pamoja na jitihada kubwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kutangaza bei elekezi, bado kuna wafanyabiashara wanauza bidhaa zao kwa bei ya juu kinyume na maelekezo ya Serikali.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea wafanyabiashara hao kupandisha bei za bidhaa.

(b) Inapotokezea wafanyabiashara wanakiuka maelekezo ya Serikali, Je, Wizara inachukua hatua gani.

(c) Ni kwa kiasi gani Wizara inazisimamia bei elekezi ili zisikiukwe na wafanyabiashara.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

44. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kumekuwa na changamoto ya kuingia moto msitu wa Ngezi takriban kila mwaka, ambapo hudhaniwa kwamba moto huo unatokana na kuwaka majani wenyewe.

(a) Je, suala hili lina ukweli kiasi gani.

(b) Je, ni hatua zipi Wizara yako inazichukua ili kuepusha changamoto hiyo kabla ya msimu wa kaskazi kufika, ambapo ndio muda wa kuungua msitu huo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

25. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwanza naomba nitowe pole kwa wanafunzi na walimu wa skuli ya Utaani na Chasasa kwa kupewa mtihani na Mwenyezi Mungu wa kuungua moto sehemu ya makaazi yao.

(a) Je, ni hitilafu gani iliyosababisha kuungua kwa jengo hilo.

(b) Je, ni wanafunzi wangapi waliojeruhiwa kwa tukio hilo.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
09 Mei, 2022. KATIBU WA BARAZA